**SIKU YA WANAWAKE DUNIANI**

***"SUKUMA MAENDELEO"***

Siku ya wanawake duniani huashimishwa kidunia tarehe 8 kila ya mwezi wa tatu kila mwaka. Ni siku ambayo wanawake wanatambuliwa kwa mafanikio yao bila kujali tofauti zao za kitaifa, kikabila, lugha, tamaduni, hali za kiuchumi, au kisiasa. Hivyo, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania unaungana na wanawake wote duniani katika kusherehekea siku hii ya adhimu ya Wanawake Duniani. Kauli mbiu ya mwaka huu ni ***"Sukuma Maendeleo"***. Kwa sababu ya kauli mbiu hii, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania unapenda kupazia sauti juu ya jitihada za wanawake watetezi wa haki za binadamu Tanzania pamoja na jitihada zingine ambazo zimechukukuliwa kuhakikisha wananwake watetezi wa haki za binadamu Tanzania wanaendelea kufanya kazi zao bila vitisho au hofu yoyote.

Kwa Tanzania, ukiukwaji wa haki za wanawake bado ni mkubwa. Baadhi ya ya matukio ya ukiukwaji wa haki za wanawake yanahusisha; ukatili wa kijinsia, haki ya urithi, haki ya kuwa na maamuzi na kuhusishwa kwenye uongozi, haki ya kumiliki mali/ardhi, haki ya kuwa na elimu bora na fursa mbali mbali za maendeleo. Ukiachilia mbali baadhi ya matukio yaliyoorodheshwa juu ya ukiukwaji wa haki za wanawake katika nchi yetu, yapo matukio mengine ya ukiukwaji wa demokrasia, haki ya kuishi, haki ya kujieleza na uhuru wa maoni. Pamoja na mazingira magumu wanayopitia wanawake, wapo baadhi ya wanawake watetezi wa haki za binadamu ambao wameendele kuwa mstari wa mbele katika kupigania ukiukwaji wa haki za binadamu Tanzania. Kwa misingi hiyo, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unapenda kuwatambua wanawake wachache ambao wamekuwa vinara wa kupigania haki za binadamu kwa mwaka 2017/2018.

1. **Mama Samia Suluhu Hassan**-Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mpiganaji wa haki za wanawake na watoto Tanzania.
2. **Halima Mdee**- Mbunge wa Kawe, mwanamke mahiri na mwanasiasa anayepigania haki za kisiasa kwa wanawake.
3. **Daktari Hellen Kijo Bisimba**- Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ambaye ni mpigania haki za binadamu mkongwe na amekuwa mstari wa mbele katika kupigania utawala wa sheria, demokrasia na uchaguzi huru na wa haki.
4. **Wakili Fatma Katume**- Wakili wa Kampuni wa Mawakili ya IMMMA; mtetezi wa haki za binadamu ambaye amekuwa akitumia taaluma yake ya sheria katika kuhakikisha heshima juu ya haki, utawala wa sheria, demokrasia, na uchaguzi huru na waki.

5. **Vicky Ntetema**- Mkurugenzi Mtendaji wa Under the same Sun, shirika la kutetea haki za watu wenye ualbino ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha watu wenye ualbino Tanzania wanaishi katika mazingira salama.
6. **Rose Sarwatt**- Mkurugenzi Mtendaji wa Umoja wa Wanawake Wajane Tanzania (TAWIA) ambaye binafsi na kwa kutumia miradi inayofadhiliwa na wafadhili amekuwa kinara wa kutetea haki za wanawake wajane Tanzania.
7. **Maria Sarungi Tsehai**- Mkurugenzi Mtendaji wa Change Tanzania; mtetezi wa haki za wanawake ambaye amekuwa wakala wa mabadiliko na kuhakikisha sauti za wasiosikika zinasikika kupitia mitandao ya kijamii.
8. **Salma Said**- Mwandishi wa Habari- Mtetezi wa haki za wanawake ambaye amekuwa akitumia mitandao ya kijamii na uandishi wa habari kuibua ukiukwaji wa haki za kisiasa na kijamii Zanzibar.
9. **Jane Magigita**- Mkurugenzi Mtendaji wa Equality for Growth; Mtetezi wa haki za Wanawake na mpigania maendeleo na uhusishwaji wa wananchi katika mambo yanayowahusu.
10. **Maanda Ngoitiko**- Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la wanawake wafugaji (PWC) vijijini ambaye pamoja na vitisho mbali mbali vya kila siku, ameendelea kutetea haki ya ardhi kwa watu wa vijijini wilaya ya Ngorongoro.

Wakati tunawatambua na kuwapongeza wanawake wakongwe wanaopigania haki za binadamu Tanzania katika nyanja mbali mbali, Mtandao unapenda pia kuwainua wanawake chipukizi wapigania haki za binadamu kama vile, **Faraja Nyalandu, Elsie Eyakuze, Rebecca Gyumi, Angela Benedicto, Carol Ndosi, Ummy Nderinago** na wengine wengi kuhakikisha wanaendelea kupigania haki za binadamu na kuwa mstari wa mbele kuhakikisha demokrasia, utawala wa sheria pamoja haki zingine za binadamu zinadumishwa kwa ajili ya kizazi cha leo na kesho.

Wakati huu tunapoadhimisha siku ya Wanawake Duniani siku ya leo tarehe 8 mwezi wa 3 mwaka 2018, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania unapenda kuwaasa wanawake watetezi wa haki za binadamu Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya yafuatayo;

- Kupaza sauti juu ya kauli mbiu ya mwaka huu juu ya *“**Sukuma Maendeleo**”*
- Kutetea haki za wanawake kwa kuwahamasisha watungaji wa sheria kuhakikisha wanatunga sheria zinazowatambua wanawake kama chachu ya maendeleo, kuzithamini kazi za mwanamke, na kuhakikisha ulinzi wa wanawake watetezi wa haki za binadamu dhidi ya madhila mbali mbali wanayopitia katika utekelezaji wa shuhuli zao. Hii itasaidia kuhakikisha ulinzi wa haki za wanawake na haki zingine kwa ujumla.
- Kupigania madabiliko ya sheria kandamizi na zenye ubaguzi ambazo zinaathiri wanawake watetezi wa haki za binadamu.
- Kuendelea kupinga ubaguzi wa kijamii, kiutamaduni, kidini, na kiuchumi ambao unapelekea wanawake kuwa katika hatari mbali mbali wakati wanatekeleza majukumu yao.
- Kufanya kazi kwa umoja na kuwa na sauti moja katika kupigania haki za wanawake. Wanawake wakiwa na sauti moja itakuwa rahisi kuongeza nafasi ya wanawake Tanzania


na kwa namna hiyo chochote wanachopigania wanawake kitaweza kusikika na kutekelezwa haraka.

- Kudumisha ushirikishwaji wa wanawake kama wadau muhimu sawa na wanaume ili kuhakikisha maendeleo endelevu, amani, usalama na kuheshimu haki za binadamu.
- Kuwawezesha wanawake kama nguzo muhimu juu ya changamoto za kuhakikisha ustawi wa kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni Tanzania.

***“Heri ya Siku ya Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu Duniani”.***
**#SukumaMaendeleo**

**Imetolewa leo tarehe 8/03/2018**

**Na: Onesmo Olengurumwa**



**Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)**